



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Kumb. Na. RDC/S.5/39 VOL.1/11

Tarehe: 10/10/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anakaribisha maombi kutoka kwa watanzania wenyewe sifa ili kuziba nafasi kama ifuatavyo:-

1) Dereva (Driver) Nafasi 2

a) Sifa za mwombaji:-

- i) Awe na elimu ya kidato cha IV
- ii) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic driving course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- iii) Awe na leseni ya udereva daraja la "E" au "C" ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- iv) Mwombaji awe na umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

b) Majukumu ya Kazi

- i) Kukagua gari kabla ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- vi) Kufanya usafi wa gari.
- vii) Kufanya kazi kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

Ngazi ya mshahara kima cha chini kwa kadri ya azimio la Baraza la Madiwani.

MASHARTI YA JUMLA

- i) Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka 18 – 45.
- ii) Waombaji wote waambatishe Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

- iii) Waombaji waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na majina matatu ya wadhamini.
- iv) Maombi yaambatishwe na picha moja (passport size) ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma.
- v) Maombi yaambatishwe na Nakala za vyeti vya taaluma/Shule na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya vyuo.
- vi) Waombaji wote waambatishe Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ambao hawana vitambulisho hivyo, namba za NIDA iandikwe kwene maelezo (CV).

2. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwa kutumia anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,

S.L.P. 148

TUKUYU.

Maombi ambayo yatawasilishwa kwa njia ya mkono hayatashughulikiwa.

NB: Tangazo hili linapatikana pia kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambayo ni www.rungwedgec.go.tz na Mbao za Matangazo za Halmashauri.

Limetolewa na:

Castory Makeula

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
RUNGWE** ~~**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**~~
RUNGWE

4. Maombi yanapokelewa kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe 24/10/2022 saa 9:30 Alasiri.